

Chaguo za Matibabu kwa Wagonjwa wa Covid-19

Matibabu ya Kupachisha Fungomwili

Matibabu ya kupachisha fungomwili ni nini?

Fungomwili zilizopachishwa ni kingamwili zinazotengenezwa maabarani. Fungomwili hizi hufanya kazi kama kingamwili asilia, ambazo ni protini zinazotengenezwa na mwili ili kukabiliana na virusi.

Fungomwili zilizopachishwa huingizwa kupitia mishipa na hupeanzwa katika vituo vya huduma za afya. Matibabu haya yanaruhusiwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Marekani (FDA) chini ya Uidhinishaji wa Matumizi ya Dharura (EUA) huku tafiti za kimatibabu zikiendelea kuchunguza manufaa na usalama wake.

Kwa nini ninapaswa kupokea matibabu ya kupachisha fungomwili?

Ukigunduliwa kuwa na COVID-19 na una dalili za ndogo hadi wastani, kupewa matibabu ya matibabu ya kupachisha fungomwili haraka iwezekanavyo kutasaidia **kupunguza** yafuatayo:

- Ukali wa dalili
- Uwezekano wa kulazwa hospitalini
- Kiasi cha virusi vinavyobebwa na mtu aliyeambukizwa

Ninapaswa kupokea lini matibabu ya kupachisha fungomwili?

Matibabu ya kupachisha fungomwili yananufaisha zaidi ikiwa yatatolewa haraka iwezekanavyo baada ya mtu kupatikana na maambukizo ya COVID-19 (ndani ya siku 10 baada ya kuanza kwa dalili).

Nani anastahiki kupewa matibabu haya?

Mtu yeyote (umri wa miaka 12 na zaidi) ambaye atatambuliwa kuwa na COVID-19 NA ana dalili ndogo hadi wastani. Pata ushauri wa mtoa huduma wako wa afya ili kubaini kama unastahiki kupokea matibabu haya. Mtoa huduma wako wa afya atahitaji kuthibitisha kuwa hakika umeambukizwa.

Ikiwa una maswali yoyote ya ziada, wasiwasi na/au unahitaji mwongozo zaidi kuhusu kuagiza matibabu au unawapa wagonjwa rufaa, wasiliana na Kituo cha Uendeshaji cha NDDoH (DOC) kupitia 701-328-0707.

Je, ni madhara gani yanayoweza kutokea kutokana na matibabu haya?

Madhara ya kawaida ni kichefuchefu, kizunguzungu, kuwashwa, na upele.

Kwa kuwa matibabu haya yanawekwa kupitia mishipa, baadhi ya watu wanaweza kupata maumivu ya muda mfupi, kuvuja damu, michubuko ya ngozi, uchungu, uvimbe na uwezekano wa kuambukizwa kwenye sehemu ya kudungwa.

Je, ninaweza kupata matibabu haya vipi na wapi?

Pata ushauri wa mtoa huduma wako wa afya akupe maagizo ya matibabu na rufaa kwenye kituo cha afya cha North Dakota ambacho hutoa matibabu ya kupachisha fungomwili.

Tazama [Ramani hii ya vituo vya huduma za afya katika jimbo la North Dakota vinavyotoa matibabu ya kupachisha fungomwili.](#)

Je, nitalipa kiasi gani kupokea matibabu haya/yanagharamiwa na bima yangu?

Serikali ya shirikisho inasambaza vifaa vya fungomwili bila kuwalipisha wagonjwa. Bima kubwa zaidi za kibinafsi hulipia gharama ya matibabu haya. Hata hivyo, ikiwa huna bima au huna uhakika, wasiliana na kituo cha matibabu ufahamu kama kuna malipo yoyote.

<https://combatcovid.hhs.gov/available-covid-19-treatment-options>

Je, ninaweza kupokea chanjo ya COVID-19 baada ya kupokea matibabu ya kupachisha fungomwili?

Bado hatujui utendakazi wa chanjo kwa mtu ambaye awali amepokea matibabu ya fungomwili kwa maambukizi ya COVID-19 au kama matibabu ya fungomwili yanaweza kutatiza mwitikio wa kingamwili yako dhidi ya chanjo. Hata hivyo, ukishakuwa na COVID-19, hakuna uwezekano mkubwa wa kuambukizwa tena katika miezi mitatu inayofuata. Ukipokea matibabu ya fungomwili, unapaswa kuchelewesha kupokea chanjo kwa siku 90 kama njia ya kujihadhari.

Vyanzo:

Matibabu ya COVID-19: Idara ya Afya ya North Dakota (<https://www.health.nd.gov/covidtreatment>)

Chaguo za Matibabu ya COVID-19: Idara ya Afya ya Minnesota
(<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/meds.html#what>)

Ikiwa una maswali yoyote ya ziada, wasiwasi na/au unahitaji mwongozo zaidi kuhusu kuagiza matibabu au unawapa wagonjwa rufaa, wasiliana na Kituo cha Uendeshaji cha NDDoH (DOC) kupitia 701-328-0707.

Ilisishwa tarehe 30/11/2021